



Adhabu


- Adelheid Marie Bwire
- Melany Pietersen
- Monica Shank Lauwo, Lauwo George
- 2
- Kiswahili sw



Siku moja, mama alileta matunda mengi.



“Tutakula matunda lini?” tunauliza. “Tutakula matunda leo jioni,” mama anasema.




Kaka yangu Rahim ni mlafi. Anaonja onja matunda yote. Anakula matunda mengi.




"Angalia Rahim alichokifanya!" mdogo wangu analalamika kwa sauti. "Rahim ni mtundu na mchoyo," ninasema.



Mama amekasirishwa na Rahim.



Sisi pia tumekasirishwa na Rahim. Lakini Rahim haombi msamaha.



"Hutamwadhibu Rahim?" mdogo wangu anauliza.



"Rahim, muda si mrefu utajuta," mama anaonya.




Rahim anaanza kuhisi kuumwa.



"Tumbo langu linauma sana," Rahim
ananong'ona.



Mama alijua hili litatokea. Matunda
yanamwadhibu Rahim!



Baadaye, Rahim anatuomba msamaha.
"Kamwe sitakuwa mlafi tena," anaahidi. Na
sote tunamwamini.



Global Storybooks

globalstorybooks.net

Adhabu

✎ Adelheid Marie Bwire

✒ Melany Pietersen

☞ Monica Shank Lauwo, Lauwo George

